## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

**Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,**

**Baraza la Madiwani.**

## TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 15/05/2023

### 1.0. UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii itagusa Maeneo yafuatayo:-

i. Taarifa ya ziara ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango katika Manispaa ya Ilemela
ii. Taarifa ya ziara ya Mhe. Jenesta Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
iii. Taarifa ya makusanyo kwa robo ya tatu.
iv. Taarifa ya fedha za mapato ya ndani zilizopelekwa kwenye miradi ya Maendeleo.
v. Taarifa ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza.
vi. Taarifa ya makabidhiano ya pikipiki 38 kwa Maafisa Ugani Kilimo.
vii. Taarifa ya Ziara ya Waheshimiwa Madiwani na Wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru



CamScanner

viii. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha kutoka Serikali Kuu kwaajili ya ukamilishaji wa Miradi ya Maendeleo

ix. Taarifa ya makabidhiano ya pikipiki 1 kwa Mtendaji wa Kata

x. Taarifa ya ziara ya Mhe. Mbunge wa Jimbo ya Ilemela

xi. Taarifa ya Halmashauri iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) Jijini Dodoma.

xii. Taarifa ya matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Manispaa ya Ilemela kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

## 2.0. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI.

i. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mnamo Tarehe 12/03/2023, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, alifanya Ziara katika Mkoa wa Mwanza na kupata fursa ya kuzungumza na wananchi wa Halmashauri yetu katika eneo la kata ya Buswelu ambapo, pamoja na mambo mengine, alisistiza umuhimu wa lishe bora kuanzia hatua za awali za ukuaji wa mtoto.

ii. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Mnamo Tarehe 20/02/2023 Mhe. Jenista Mhagama (MB), Waziri wa Nchi ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora alifika katika Halmashauri yetu kwa ajili ya kukagua miradi inayotekelezwa na TASAF III katika Kata ya Kitangiri ambapo alifanikiwa kukagua maendeleo ya Ujenzi wa Zahanati ya Mihama.

iii. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Hadi kufikia 31 Machi mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya TSh.12,189,314,578.00 sawa na asilimia 90 ya makisio ya bajeti ya mwaka 2022/2023 ambayo ni mapato ya ndani, kati ya hayo mapato halisi ni Tsh. 11,943,338,632.00 sawa na asilimia 92 ya bajeti

iv. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa robo ya tatu, kiasi cha shilingi **1,556,215,012.5** zilielekezwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ufuatao:

**Elimu Msingi**

Tumepeleka fedha kama ifuatavyo;

- Shilingi 29,194,000.00 kwa ajili ya utengenezaji wa madawati katika shule ya msingi Kahama
- Shilingi 429,000.00 kwa ajili ya malipo ya mafundi katika ujenzi wa bweni la watoto wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Buswelu.
- Shilingi 16,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Nyamhongolo
- Shilingi 20,440,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Bujingwa.
- Shilingi 587,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa vyoo shule ya msingi Ihalalo
- Shilingi 28,257,000.00 kwa ajili ua ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 7 na ofisi 2 Shule ya Msingi Shibula
- Shilingi 15,000,000.00 ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika shule ya msingi Shibula
- Shilingi 21,200,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Buyombe katika Kata ya Kahama

**Jumla ya Fedha zote Elimu Msingi ni Tsh. 131,107,000.00**

**Elimu Sekondari**

- Shilingi 30,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara ya sayansi pamoja na choo Shule ya Sekondari Buzuruga Tshs. 30,000,000.00

**Jumla ya fedha zote Elimu Sekondari ni Tshs. 30,000,000.00**

**Afya**

Tumepeleka fedha kama ifuatavyo;

- Shilingi 8,853,275.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la RCH Zahanati ya Nyamhongolo
- Shilingi 12,018,500.00 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na malipo ya fundi katika Hospitali ya Wilaya
- Shilingi 30,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa wodi ya kina mama katika Kituo cha Afya Buzuruga
- Shilingi 23,611,750.00 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la RCH Zahanati mpya ya Kawekamo

**Jumla ya fedha zote Afya ni Tsh. 74,483,525.00**

**Utawala**

Tumepeleka fedha kama ifuatavyo;

- Shilingi 225,460,984.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Jengo la Utawala
- Shilingi 15,077,075.00 kwaajili ya ukamilishaji wa Ofisi ya Mtaa wa Buzuruga Kaskazini
- Shilingi 5,000,000.00 kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Mecco
- Shilingi 37,000.00 kwa ajili ya usajili wa pikipiki 1

**Jumla ya fedha zote Utawala ni Tsh. 245,575,059.00**

**Biashara Viwanda na Uwekezaji**

Tumepeleka fedha kama ifuatavyo;

- Shilingi 58,548,550.00 kwa ajili ya uzalishaji kwenye Mradi wa Tofali
- Shilingi 11,236,128.00 kwa ajili ya gharama za uendeshaji Stendi ya Nyamhongolo
- Shilingi 10,826,928.00 kwa ajili ya ujenzi wa matundu 6 ya vyoo Soko la Kitangiri
- Shilingi 5,195,925.00 kwa ajili ya kufanya ukarabati Soko la Kirumba

**Jumla ya fedha yote Biashara Viwanda na Uwekezaji ni Tsh. 85,807,531.00**

**Miundombinu, Maendeleo ya Miji na Vijiji**

- Shilingi 3,510,000.00 kwa ajili ya Ujenzi wa barabara ya Kazamoyo mtaa wa Ibanda kata ya Kirumba
- Shilingi 3,092,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya iendayo Shule ya Sekondari Semba
- Shilingi 16,063,080.00 kwa ajili ya ukarabati wa standi ya daladala ya Buzuruga Tshs. 16,063,080.00
- Shilingi 964,000.00 kwa ajili ya ufungaji umeme wa njia tatu(3 phase) katika jukwaa -uwanja wa Furahisha

**Jumla ya fedha yote Miundombinu, Maendeleo ya Miji na Vijiji ni Tsh. 23,629,080.00**

**Mipango miji**

Tumelipa fidia kama ifuatavyo;

- Shilingi 70,889,823.25 zimetumika kulipa fidia kwenye maeneo ya shule za Sekondari za Nyamhongolo, Nyasaka, na Bujingwa
- Shilingi 709,638,243.00 zimetumika kulipa fidia ya wananchi eneo la mradi Nyafula

**Jumla ya fedha yote iliyopelekwa kwenye fidia ya ardhi ni Tshs. 780,528,066.25**

**Taarifa ya Mradi wa Viwanja Nyafula**

- Viwanja vilivyopimwa ni **3254**
- Viwanja ambavyo havijauzwa ni **141** vyenye thamani ya Tshs. **9,979,546,526.00**
- Mapato kutokana na mauzo ya viwanja hadi sasa ni Tshs. **6,456,543,715.55**
- Fedha zinazodaiwa kwa waliochukua viwanja na hawajakamilisha ni Tshs. **8,543,456,284.4**



CamScanner

**Maendeleo ya Jamii**

- Kwa kipindi hiki, Shilingi **100,000,000.00** zilitengwa kwaajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Fedha hizo hazikuweza kugawiwa kwenye vikundi kutokana na **maelekezo** ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Kassim ya kusitisha Halmashauri kuendelea kutoa mikopo hiyo kwa vikundi.

**Kilimo Mifugo na Uvuvi**

Tumepeleka fedha kama ifuatavyo;

- Shilingi 14,194,928.00 kwa ajili ya kuwezesha Matengenezo ya mzani Mwaloni

**Jumla Ndogo Kilimo Mifugo na Uvuvi Tshs. 14,194,928.00**

v. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Jumla ya wanafunzi 12,666 wakiwemo wavulana 6,184 na wasichana 6482 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 katika shule zetu za sekondari. Jumla ya wanafuzi 1,668 wakiwepo wasichana 859 na wavulana 809 wamehamia katika shule zetu. Hadi kufikia 31 Machi 2023, jumla ya wanafunzi 13,317 wa kidato cha kwanza wakiwemo wavulana 6,486 na wasichana 6,831 wameripoti katika shule za sekondari.

vi. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Mnamo Tarehe 06/02/2023 Halmashauri yetu ilipokea jumla ya pikipiki 38 kutoka Serikali Kuu kupitia Wizara ya Kilimo kwaajili ya Maafisa ugani wa Divisheni ya Kilimo ambapo Tarehe 8/02/2023 Afisa Tawala wa Wilaya ya Ilemela aligawa pikipiki hizo kwa Maafisa Ugani 38 wa Manispaa yetu.

vii. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo tarehe 11/01/2023 Wahe, Madiwani na Wataalam kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, walifika katika Halmashauri yetu ambapo walibadilishana uzoefu juu ya masuala

mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa mapato, usafi wa mazingira na pia walipata fursa ya kutembelea Stendi ya Mabasi na maegesho ya Malori Nyamhongolo.

viii. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mnamo Mwezi Machi 2023 Halmashauri yetu ilipokea Jumla ya Tshs. 140,000,000.00 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi mbalimbali, ambapo Tshs. 30,000,000.00 ni kwa ajili ya ukamilishaji wa Maabara 1 ya sayansi Shule ya Sekondari Angelina Mabula, Tshs. 30,000,000.00 ni kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara 1 ya sayansi Shule ya Sekondari Kisundi, Tshs. 30,000,000.00 ni kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara 1 ya sayansi Shule ya Sekondari Kirumba, Tshs. 30,000,000.00 ni kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara 1 ya sayansi Shule ya Sekondari Kabuhoro, na Tshs. 20,000,000.00 ni kwa ajili ya ukamilishaji wa bweni 1 Shule ya sekondari Sangabuye.

ix. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mnamo Tarehe 14 Februari 2023 Halmashauri yetu ilipata mgao wa pikipiki 1 kutoka Serikali Kuu ambapo tarehe 7 Machi 2023 pikipiki hiyo ilikabidhiwa kwa Mtendaji wa Kata ya Ilemela ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

x. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo Tarehe 18 Februari 2023 Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela Dkt. Angelina Sylivester Mabula alifanya ziara katika jimbo lake ambapo alikagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara ya Kahama- Shibula ya km 2.5, ujenzi wa bweni la wasichana katika sekondari ya Igogwe, Barabara ya Zege ya mita 180 kuelekea mwalo wa Igombe, na ujenzi wa Zahanati ya Mihama.

xi. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mnamo mwezi Januari 2023 Halmashauri iliwasilisha Taarifa ukaguzi maalim (special audit) ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mbele ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) Jijini Dodoma.



CamScanner

*Mheshimiwa Mwenyekiti,* Mnamo mwezi Machi 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitoa taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo katika taarifa hizo, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepata **HATI SAFI**.

*Mheshimiwa Mweyekiti,* naomba kuwasilisha.

Eng: Modest J. Apolinary
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**